

Na: 13. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Februari 1-10, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 11-20, 2018

MUHTASARI


- Mvua za Msimu ziliendelea vizuri katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua ambapo wakulima waliendelea na shughuli za palizi.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua waliendelea na shughuli za uvunaji wa mazao isipokuwa katika mkoa wa Shinyanga ambapo mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.
- Takriban hekta 7,144 cha mazao ya mtama na uwele yaliathiriwa na ndege aina ya kwelea kwelea katika mkoa wa Shinyanga.
- Mvua zinazotarajiwa kwa kipindi cha Februari 11-20 zitasaidia ukuaji wa mazao na malisho kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2018**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu kidogo na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kubaki Tanzania hususan katika menea ya nyanda juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi, hali hii ilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la bahari katika Bahari ya Hindi liliendelea kuwa chini ya wastani hadi wastani na kusababisha maeneo ya pwani kuwa na vipindi kadhaa vya mvua na radi hususan katika ukanda wa pwani ya kusini. Kwa upande mwingine kumekuwepo na joto la bahari la juu kidogo ya wastani hadi wastani katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) hali iliyosababisha kupunguza kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi.

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI
CHA FEBRUARI 1-10, 2018**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa iliyokuwepo kwa kipindi hicho, baadhi ya maeneo yanayopata mvua za msimu mmoja; mikoa ya Tabora, Songwe, Mbeya, Mtwara na upande wa kusini mwa mkoa wa Ruvuma yalipata mvua za wastani hadi juu ya wastani (zaidi ya 80% ya wastani wa muda mrefu kwa kipindi cha siku kumi) kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu za wastani hadi juu ya wastani zilinyesha katika baadhi ya maeneo ya Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga na Lushoto. Maeneo ya nchi yaliyosalia yalipata mvua za chini ya wastani wa asilimia 80 ya wastani wa muda mrefu kwa kipindi cha siku kumi.



Kielelezo. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha Tarehe 11-20 Februari, 2018.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2018**

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua uvunaji wa mazao unaendelea isipokuwa katika mkoa wa Shinyanga ambapo mazao yapo katika hatua ya kukomaa. Hata hivyo, hekta takriban 7,144 za mazao ya mtama na uwele yameshambuliwa na ndege aina ya Kwelea Kwelea kama ilivyotaarifiwa na Afisa Kilimo wa Mkoa wa Shinyanga. Hali ya maji na malisho ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi isipokuwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Arusha hususan katika wilaya ya Longido.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya Nyasa na Rukwa kutokana na mvua zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018

Migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo wakati migandamizo mikubwa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo. Ukanda wa mvua wa ITCZ utaendelea kubaki chini hususan katika maeneo ya nyanda juu kusini magharibi pamoja na maeneo ya kusini ambapo itapelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa mvua katika ukanda wa pwani pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuwepo kwa joto la juu ya wastani hadi wastani na hivyo kuchangia kupungua kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara), pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Maeneo hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu), magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya) na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi kadhaa vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018

Mvua zinazotarajiwa zitaendelea kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya ukuaji wa mazao katika maeneo yanayopata mvua katika msimu mmoja. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizo kwa shughuli za kilimo na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi wakati wa upungufu wa maji. Katika maeneo yanayopata mvua kwa misimu miwili kwa mwaka mvua hizi za nje ya msimu wa vuli zinatarajiwa kuimarisha ustawi wa malisho ya mifugo na upatikanaji wa maji katika maeneo hayo. Hata hivyo, mvua hizo zinaweza kuathiri mazao yaliyokomaa na shughuli za uvunaji. Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma, ziwa Tanganyika na bonde la kati kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kufuata kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza - Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz;

Tovuti: www.meteo.go.tz